

# »Kutengeneza jukwaa la kondoo na mbuzi lililoinuliwa«

Watu wengi ulimwenguni hufuga kondoo kwa kutoa nyama, sufu na maziwa. Katika mabanda ya kijadi, kondoo na mbuzi mara nyingi hufugwa wakiwa chini ambalo huwaweka wanyama hao katika mgusano wa moja kwa moja na mkojo pamoja na kinyesi chao. Hii husababisha usafi duni ambao hufanya wanyama wengi kupata magonjwa.

Ili kutatua changamoto hii, unaweza kuandaa jukwaa lililoinuliwa ndani ya banda lililopo ambalo linaweza kusafishwa chini yalo kwa urahisi. Jukwaa lililoinuliwa hupunguza uwepo wa magonjwa, na ni rahisi kusafisha banda, na unaweza pia kutengeneza mbolea kutoka kwa samadi.

## kujenga jukwaa

Vipimo vya jukwaa huchukuliwa, miguu ya jukwaa hujengwa. Kutegemea urefu wa banda, mianzi hukatwa kwa urefu unaohitajika kufanya vizingi vya kushikilia au kuimarisha jukwaa ili kuwezesha ukusanyaji rahisi wa samadi. Ikiwezekana, jukwaa linapaswa kuwa angalau lm juu ya ardhi.

Kata kipengo kwenye pande ya mwisho wa kigingi. Chimba shimo la kina cha nusu mita likiwa karibu na pembe ambapo unataka kuweka vizingi. Kulingana na ukubwa wa jukwaa, utahitaji kuweka vizingi vingine katikati, kila kigingi kinapaswa kuwa mita lm mbali na kingine, na lazima vyote viwe thabiti na ngangari.

Vijiti vya mianzi huwekwa kimlalo juu ya vizingi na kufungwa kwenye kipengo kilicho katika vizingi. Mianzi iliyonyooka huchaguliwa ili kutengeneza mbao za sakafu. Mianzi hukatwa kulingana na upana wa banda.

## **Kupunguza uwepo wa hatari**

Vifundo vikali hutolewa na husawazishwa ili wanyama wasiumizwe. Kila kijiti cha mianzi hupasuliwa katika vipande vinne sawa. kingo zilizo na ncha kali hutolewa na kusawazishwa ili kulainisha vipande vilivyopasuliwa ambavyo huwekwa juu ya vijiti vya mianzi vilivyowekwa awali kimlalo. Vipande hivyo hutundikwa kwa kila upande wa jukwaa ili kuandaa sakafu.

Kutoka kwenye vipande vilivyotundikwa, vingine hufungwa na kamba vikielekea katikati, kwa njia ambayo vinaweza kukunjwa kwa hivyo kuwezesha banda kusafishwa kwa urahisi. Mapengo hayapaswi kuachwa kati ikiwa unatumia mianzi mbichi. Ngazi ya mifuko ya mchanga hutengenezwa ili kusaidia kondoo na mbuzi kuingia na kutoka.

Jukwaa linapaswa kusafishwa kila siku ili wanyama wawe na afya.